

## **Sera ya Matumizi Yanayofaa ya Wilaya ya Shule ya Granite Makubaliano ya Matumizi ya Teknolojia Inayotumiwa na Mwanafunzi**

Matumizi ya teknolojia yanaweza kuwa na faida kwa elimu ya mwanafunzi. Matumizi ya teknolojia inayomilikiwa na Wilaya na ufikiaji wa Intaneti ya shule ni fadhila, ambayo inaweza kuruhusiwa na vile vile kuondoshwa. Wanafunzi wanatarajiwa kufahamu na kuzingatia yafuatayo:

### **1. Usalama wa Mwanafunzi Binafsi**

Maelezo binafsi ya namna ya kuwasiliana na mwanafunzi hayawezi kuingizwa kwenye kurasa za Intaneti ambazo zinatumiwa na umma. Hii ni pamoja na anwani ya mwanafunzi, nambari za simu, anwani binafsi ya barua pepe na maelezo mengine ya mtu binafsi.

### **2. Matarajio ya Ufaragha**

Wanafunzi wasitarajie ufaragha katika faili, diski, hati, barua pepe n.k. ambazo zimetumiwa au kutayarishwa na vifaa vya Wilaya.

### **3. Faragha ya Data za Mwanafunzi**

Sheria ya jimbo la Utah inahitaji kila shule wilayani kufichua inashiriki maelezo ya mwanafunzi na wahusika gani wa tatu. GSD hutangaza maelezo haya katika ukurasa wao wa mtandao wa teknolojia wa kimasomo chini ya kichupo cha Taarifa za *Faragha ya Data za Mwanafunzi*.

<http://academictechnology.graniteschools.org/studentdataprivacy.aspx>

*Programu inayoshirikisha habari za mwanafunzi ambazo walimu wanwaeza kuwa wakitumia zinaweza kupatikana katika tovuti ya Ripoti ya Matumizi ya*

*Wilaya.*[http://academictechnology.graniteschools.org/usage\\_reporting.aspx](http://academictechnology.graniteschools.org/usage_reporting.aspx)

### **4. Matumizi Yaliyopigwa Marufuku ya Kompyuta na Vifaa**

Wanafunzi **wamekatanzwa** kufanya yafuatayo (sio orodha kamili) –

Kufikia, kuhifadhi au kutengeneza faili/programu zenye matusi, lugha chafu, au za kiponografia  
Kuiba maandishi au mawazo ya watu wengine bila kukiri kuwa ni yao au kukiuka sheria za hakimiliki au nembo

Kuharibu, kugeuza, au kurekebisha vifaa vya maunzi au programu zinazomilikiwa na Wilaya

Kujaribu kukwepa mfumo uliowekwa wa kulinda kompyuta

Kupakua na kutumia programu ambazo hazijaidhinishwa

Kuumiza, kuchafulia mtu jina, kunyanyasa, au vinginevyo kudhalimu watu WOWOTE kwa njia ya mtandao

Matumizi ambayo hayajaidhinishwa masomo yanapoendelea darasani

### **5. Matumizi ya Intaneti**

Wanafunzi wanaweza kutumia huduma ya intaneti ya shule wakati ambapo wameidhinishwa kufanya hivyo tu.

## 6. Hatua za Kinidhamu

Hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa mujibu wa makubaliano haya (k.m., kutokuwa na idhini ya kutumia vifaa hivyo tena, kusitisha masomo kwa muda, kushirikishwa kwa maafisa wa polisi, n.k.).

*Ili kupata taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mwanafunzi wako au usimamizi wa shule yao.*

Jina la Mwanafunzi (La Kwanza) \_\_\_\_\_ (Herufiya Kwanza ya Jina la  
Katikakti) \_\_\_\_\_ (La Mwisho) \_\_\_\_\_  
(Tafadhali Chapisha)

Darasa \_\_\_\_\_ # ya Mwanafunzi # \_\_\_\_\_

**Iwapo nitapata fursa ya kutumia vifaa vya kompyuta vya Wilaya, nitavitumia kulingana na masharti ya Makubaliano ya Matumizi ya Teknolojia ya Wanafunzi.**

Saini ya Mwanafunzi \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

**Ninampa idhini mtoto wangu kutumia teknolojia ya Wilaya na intaneti kulingana na masharti ya Makubaliano haya.**

Saini ya Mzazi/Mlezi \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_